

Doris Stephen Mathew,
Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto(IJA)
S.L.P 20,
Simu: 0766853157 / 0692200016
LUSHOTO – TANGA.
04/01/2024

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Utumishi,
S.L.P 670, **DODOMA.**

**YAH: UHAMISHO KURUDI KWA MWAJIRI WA AWALI (BI. DORIS S. MATHEW –
CHEKI NA. 111702186)**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu Pamoja na barua yako yenye Kumb. Na.CA.178/311/01/S/122 ya tarehe 1/12/2023 kuhusu kurudi kwa mwajiri wa awali Halmashauri ya Monduli.

Ikumbukwe mnamo mwezi Julai, 2022 kupitia barua yenye Kumb. Na. CA.178/311/01/L/91 ya tarehe 11 Julai, 2022 nilipata uhamisho kutoka Halmashauri ya Monduli ambapo nilikuwa mtumishi katika kada ya Ualimu (Msingi) kwenda Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA) Tanga ambapo hadi sasa nimetumikia kama Afisa Mtihani Daraja la II kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na miezi 6.

Ninaomba ofisi yako inisaidie niweze kupangiwa kituo kingine cha kazi hususani ndani ya Mkoa wa Dodoma ili niweze kuendelea kuhudumu kama Afisa Mtihani Daraja la II Kwani ninamatatizo ya kiafya ambayo nadhani kwa kurudi kwangu kwenye kada ya ualimu inaweza kunitea shida zaidi kwani siwezi kusimama kwa muda mrefu na pia siwezi kutembea umbali mrefu, pamoja na hali ya hewa ya baridi. Hata hivyo bado nipo kwenye mchakato wa matibabu Kwani mpaka sasa nimefanyiwa operasheni moja ya mguu wa kulia bado mwingine na ninatakiwa kuhudhuria kliniki mara kwa mara hivyo basi ninaomba kusaidiwa ili niweze kuwa katika mazingira ambayo ya takuwa salama kwa afya yangu. Pia kurudi katika kituo cha awali kutaathiri morali yangu ya kazi kwani tayari nilishaweza kumudu kazi zangu za Afisa Mtihani daraja II ambayo nimeifanya kwa mwaka na nusu na niliweza kufanya kwa uaminifu na kwa weledi wa hali ya juu.

Hivyo, kwa heshima na taadhima na kwa mamlaka uliyonayo ninaomba kufikiriwa ombi langu la kuhamishiwa taasisi nyingine ambayo ipo katika mkoa wa Dodoma ili niweze kutibiwa kwa urahisi zaidi na pia niweze kuhudhuria kliniki kwa urahisi zaidi tofauti na ninavyo safari kutokana na changamoto za magoti. Pia niweze kuwa karibu na familia yangu, ili iweze kunisaidia katika changamoto ya afya nliyonayo. Pamoja na barua hii, ninaambatisha barua mbili za uhamisho wa awali na wa sasa pamoja na taarifa ya Daktari kwa ajili ya rejea.

Ni matumaini yangu ombi langu litafikiriwa.

Wako Mtiifu,



Doris Stephen Mathew

(Afisa Mtihani Daraja la II)

Cheki Na.111702186

Nakala: Mkuu wa chuo,

Chuo cha uongozi wa mahakama IJA,
S.L.P 20,
Lushoto